# SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR

## WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

## MUHTASARI WA HISABATI
### KWA ELIMU YA MAANDALIZI ZANZIBAR

### TAASISI YA ELIMU ZANZIBAR

### 2012

© Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, 2012

Haki zote zimehifadhiwa, hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa, maandishi nukta nundu na kutoa Muhtasari huu kwa jinsi yoyote ile bila ya idhini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Umetayarishwa na:
Taasisi ya Elimu Zanzibar
S.L.P. 840
**Zanzibar**

# YALIYOMO

**Ukurasa**

YALIYOMO ........ ii
Utangulizi: ........ iii
Ujuzi wa Jumla wa Somo la Hisabati ........ iii
Malengo ya Jumla ya Somo la Hisabati ........ iv
MUHTASARI WA HISABATI KWA MWAKA WA KWANZA ........ 1
MWAKA WA PILI ........ 11

# HISABATI

## Utangulizi:

Somo hili ni muhimu katika kukuza vipaji vya kufikiri, kulinganisha, kupembua na kufananisha pamoja na kukuza stadi za kusoma. Vile vile vitendo vya Hisabati vinawajengea watoto uwezo wa kukabili vyema mawazo dhahania kwa siku za baadae.

### Ujuzi wa Jumla wa Somo la Hisabati

Baada ya kujifunza somo la Hisabati katika skuli za Maandalizi, watoto wataonesha ujuzi wa:-

1. Kuweka vitu pamoja kulingana na sifa za vitu zikiwemo rangi, umbo, ukubwa, uzito na hali.
2. Kupanga vitu kwa mtiririko wa kimo, uzito, urefu, ugumu, umbo na rangi.
3. Kutumia dhana ya wakati, nafasi, mwendo wa kasi na ujazo.
4. Kusoma, kuhesabu, kufanya hesabu za kujumlisha na kutoa.
5. Kutumia dhana za kihesabati katika maisha yao ya kila siku.
6. Kulinganisha vitu kwa sifa zake.
7. Kuainisha na kutumia sarafu.
8. Kupanga nambari na thamani yake kwa nambari 1 – 20.
9. Kujumlisha na kutoa nambari jawabu yake isiyozidi 10.

## Malengo ya Jumla ya Somo la Hisabati

Somo la Hisabati linafundishwa katika skuli za Maandalizi ili watoto waweze:-

1. Kufahamu sifa za vitu zikiwemo rangi, umbo, ukubwa, uzito na hali.
2. Kuelewa upangaji wa vitu kwa mtiririko wa kimo, uzito, urefu, ugumu, umbo na rangi.
3. Kutambua dhana ya wakati, nafasi, mwendo wa kasi na ujazo.
4. Kujua kuhesabu nambari 1 – 100.
5. Kuthamini dhana za hesabati katika maisha yao ya kila siku.
6. Kusoma nambari, kuhesabu vitu na kufanya hesabu za kujumlisha kwa nambari 1 – 100.
7. Kuelewa uwekaji wa vitu pamoja kulingana na sifa zao zikiwemo rangi, umbo, ukubwa, uzito na hali.
8. Kutambua ulinganishaji wa vitu kwa sifa zake.
9. Kutambua thamani ya nambari 1 -20.
10. Kuelewa sarafu na matumizi yake.
11. Kuelewa ujumlishaji na utoaji wa hesabu ndogo ndogo.

# MUHTASARI WA HISABATI KWA MWAKA WA KWANZA

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| 1.MAUMBO<br>(a) Maumbo Bapa | Mtoto aweze kuanisha maumbo bapa. | 1. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze watoto kuainisha maumbo bapa.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya kuchora, mwalimu awaongoze watoto kuainisha maumbo bapa.<br>3. Kwa kutumia mbinu ya mchezo, mwalimu awaongoze watoto kuainisha maumbo bapa. | 1. Kadi za maumbo bapa.<br>2. Chati za maumbo /chati mguso.<br>3. Chati za maumbo yaliyokatwa.<br>4. Fulana bodi | 9 |
| (b) Aina za Maumbo Bapa | (i) kutaja baadhi ya maubo bapa. | 1. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze watoto kutaja maumbo bapa. | 1. Kadi za umbo bapa la duara, sambusa na kashata.<br>2 Chati mguso za maumbo bapa. | 9 |
| | (ii) Kupanga maumbo bapa kutokana na aina zake. | 1. Kwa kutumia mbinu ya kumechisha, mwalimu awaongoze watoto kupanga maumbo bapa kwa mujibu wa aina zake. | 1. Kadi za umbo bapa la duara, sambusa na kashata. | |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | 2. Kwa kutumia mbinu ya mchezo, mwalimu awaongoze watoto kuainisha maumbo bapa. | | |
| 2. KUPEMBUA NA KUPANGA<br>(a) Hali ya Vitu na Sifa zake | Mtoto aweze Kutenganisha vitu mbali mbali kulingana na sifa zake. | 1. Kwa kutumia mbinu ya kuonesha, mwalimu awaongoze watoto kutenganisha vitu mbali mbali kulingana na sifa zake (rangi na maumbile yake)<br>2. Kwa kutumia mbinu ya mchezo , mwalimu awaongoze watoto kutenganisha vitu mbali | Vitu mbali mbali vyenye hali tofauti. | 3 |
| | | mbali kulingana na sifa zake<br>3. Kwa kutumia mbinu mbinu ya kuchora mwalimu awaongoze watoto kulinganisha vitu kwa urefu na ufupi.<br>4. Kwa kutumia mbinu ya kusimulia hadithi mwalimu awaongoze watoto kulinganisha vitu kwa urefu na ufupi. | | |
| (b) Eneo | Mtoto aweze:- | 1. Kwa ktutumia mbinu ya kuchora | 1. Kadi za maubo bapa. | 9 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | (i) kuanisha eneo. | na kupaka rangi, mwalimu awaongoze watoto kuainisha eneo la umbo bapa.<br>2. Kwa ktutumia mbinu ya kucheza, mwalimu awaongoze watoto kuainisha eneo kwenye mazingira kwa kuzungusha uzio.<br>3. Kuainisha eneo kwenye mazingira kwa kuzungusha uzio | 2. Penseli za rangi.<br>1. Mbao ndogo ndogo<br>2. Kamba<br>3. Vijiti vya uzio. | |
| | (ii) Kulinganisha maeneo. | 1. Kwa kutumia mbinu ya kusimulia hadithi, mwalimu awaongoze watoto kulinganisha maeneo makubwa na madogo.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya onyesho, mwalimu awaongoze watoto kulinganisha maeneo ya vitu.<br>3. Kwa kutumia mbinu ya matembezi, mwalimu awaongoze watoto kulinganisha maeneo makubwa na madogo. | 1. Chati za ramani/chati mguso za ramani.<br>2. Mbao ndogo ndogo na kubwa.<br>3. Kadi za mialiko kubwa na ndogo. | . |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| (c) Uzito. | Mtoto aweze:-<br>Kulinganisha vitu kwa uzito na wepesi. | 1. Kwa kutumia mbinu ya utabiri na majaribio mwalimu awaongoze watoto kutabiri vitu vizito baadaye wathibitishe utabiri wao kwa majaribio<br>2. Kwa kutumia mbinu ya maonyesho mwalimu awaongoze watoto kulinganisha vitu kwa uzito na wepesi. | Vitu mbali mbali uzito na vyepesi, mizani | 8 |
| (d) Ujazo. | Mtoto aweze:-<br>(i) Kupima ujazo wa vitu tofauti. | 1. Kwa kutumia mbinu ya mchezo mwalimu awaongoze watoto kupima ujazo wa vitu tofauti<br>2. Kwa kutumia mbinu ya uchunguzi mwalimu awaongoze watoto kujaza vitu kwa ujazo tofauti.<br>3. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kupima ujazo wa vitu tofauti. | 1. Maji.<br>2. Chupa za plastic.<br>3. Unga wa mbao.<br>4. Vikopo.<br>5. Mchanga | 9 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kulinganisha | Kwa kutumia mbinu ya onesho , mwalimu awaongoze watoto kuonesha vitu vyenye ujazo tofauti (uliojaa,usiojaa), | 1. Chati inayoonesha ujazo wa vitu/chati mguso<br>2. Maji.<br>3. Mchanga.<br>4. Chupa za plastic.<br>5. Vikopo.<br>6. Unga wa mbao | |
| 4. WAKATI<br>(a) Ratiba ya Siku. | Mtoto aweze:-<br>Kutaja matendo anayoyatenda kwa siku. | 1. Kwa kutumia mbinu ya nyimbo mwalimu awaongoze watoto kutaja matendo anayoyatenda kila siku.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kutaja matendo anayoyatenda kwa siku kuanzia asubuhi anapoamka mpaka anapolala.<br>3. Kwa kutumia mbinu ya igizo mfano mwalimu awaongoze watoto kutaja matendo | 1. Chati<br>2. Kadi ndogo ndogo zinazoonesha vitendo vya siku.<br>3. Saa bandia<br>4. Saa halisi/chati inayoonesha matendo ya siku | 6 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | anayotenda kwa siku. | | |
| (b) Siku za Wiki | Mtoto aweze:-<br>Kutaja katika wiki kwa mpango siku zilizomo. | 1. Kwa kutumia mbinu ya nyimbo mwalimu awaongoze watoto kutaja siku zilizomo katika wiki kwa mpango<br>2. Kwa kutumia mbinu ya kuonesha, mwalimu awaongoze watoto kutaja siku zilizomo katika wiki kwa mtiririko. | 1. Chati inayoonesha siku za wiki/mguso<br>2. Kadi ndogo ndogo/mguso<br>3. Radio.<br>4. CD | 6 |
| | | 3. Kwa kutumia mbinu ya kumechisha, mwalimu awaongoze watoto kutaja siku zilizomo katika wiki kwa mpango. | | |
| (c) Mtiririko wa Matukio. | Mtoto aweze:<br>Kutaja mtiririko wa matukio.. | . 1. Kwa kutumia mbinu ya nyimbo mwalimu awaongoze watoto kutaja mtiririko wa matukio wanayoyatenda kwa wiki.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze | 1. Chati ya siku za wiki.<br>2. Sinema. Box<br>3. Kadi za siku | 6 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | watoto kutaja mtiririko wa matukio wanayoyatenda katika wiki. | | |
| 5. NAMBARI<br>(a) Kuhesabu 1 – 50 | Mtoto aweze:-<br>(i) Kuhesabu nambari 1 – 50 (kwa awamu) | 1. Kwa kutumia mbinu ya nyimbo, mwalimu awaongoze watoto kuhesabu nambari 0 – 50 .<br>2. Kwa kutumia mbinu ya onesho mwalimu awaongoze watoto kuhesabu nambari 0 – 50 kwa kwa mtiririko.<br>3. Kwa kutumia mbinu ya mchezo mwalimu awaongoze watoto kuhesabu nambari 0 – 50. | 1. Chati za nambari/ mguso<br>2. Vifaa mbali mbali vya kuhesabia<br>3. kadi za samaki wa kuvua.<br>4 Kadi za nambari/mguso<br>5. Abakasi | 14 |
| | (ii) Kupanga nambari | Kwa kutumia mbinu ya mchezo walimu awaongoze watoto kupanga nambari kwa mtiririko. | 1. Kadi za nambari | |
| (b)Kusoma Nambaari 1—50 | Mtoto aweze :-<br>(i) kusoma nambari 1—50 (kwa awamu) | Kwa kuutumia mbinu ya maonyesho, mwalimu awaongoze wanafunzi kusoma nambari. | Kadi za numerali. | 6 |
| (c) Kuandika Nambari 0 - 50 | Mtoto aweze Kuainisha thamani ya | 1. Kwa kutumia mbinu ya nyimbo mwalimu awaongoze watoto | 1. Chati ya nambari na thamani | 20 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | nambari. | kuainisha thamani ya nambari.<br>2. Kwa kutumia mbinu onesho mwalimu awaongoze watoto kuainisha thamani ya nambari.<br>3. Kutumia mbinu ya kumechisha mwalimu awaongoze watoto kuainisha thamani ya nambari | yake/mguso<br>2. Vifaa mbali mbali vya kuhesabia.<br>.3. Kadi za nambari<br>4. Abakasi | |
| (d) Nambari na thamani yake (0 – 10) | Mtoto aweze Kujumlisha na kutoa. | 1. Kwa kutumia mbinu ya onesho mbinu mwalimu awaongoze watoto kutoa na kujumlisha vitu.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya mazoezi, mwalimu awaongoze watoto kujumlisha na kutoa vitu mbali mbali (jawabu isizidi kumi). | 1. Vifaa mbali mbali vya kuhesabia.<br>2. Chati/chati mguso<br>3. kadi za nambari<br>4. karatasi<br>5. Mabuku na penseli. | 12 |
| (e) Matendo ya Kihesabati | Mtoto aweze :-<br>(i) kujimlisha nambari (jibu lisilozidi kumi) | 1. Kwa kutumia onyesho mbinu, mwalimu awaongoze watoto kujumlisha vitu<br>2. Kwa kutumia mbinu ya mazoezi, mwalimu awaongoze watoto kujimlisha vitu mbali mbali ( | 1. Vifaa mbali mbali vya kuhesabia<br>2. Chati/ chati mguso<br>3. Kadi za namabri.<br>4. karatasi | 12 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | jawabu lisizidi kumi bila ya kuandika nambari) | 5. aamabuku na penseli.<br>6. Abakasi | |
| | (ii) Kutoa nambari (jibu lisilozidi kumi) | 1. Kwa kutumia onyesho mbinu mwalimu awaongoze watoto kutoa vitu.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya mazoezi mwalimu awaongoze watoto kutoa vitu mbali mbali (nambari ya kutoa na kutolewa isizidi kumi)<br>3. Bila kuandika nambari | 1. Vifaa mbali mbali vya kuhesabia.<br>2. Chati/chati mguso<br>3. kadi za nambari<br>4. Karatasi<br>5. Mabuku na penseli<br>6. Abakasi | |
| 6. FEDHA<br>(a) Sarafu. | Mtoto aweze:<br>(i) Kutaja aina za sarafu. | Kwa kutumia mbinu ya kuonesha, mwalimu awaongoze watoto kutaja aina za sarafu. | 1. Sarafu halisi.<br>2. Chati/chati mguso<br>3. sarafu bandia.<br>4. Vitu mbali mbali vinavyohusiana na duka. | 7 |
| | (ii) Kutumia sarafu | 1. Kwa kutumia mbinu ya mchezo | 1. Sarafu bandia. | |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | mwalimu awaongoze watoto kutumia sarafu.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kutumia sarafu.<br>3. Kwa kutumia mbinu ya hadithi mwalimu awaongoze watoto kutumia sarafu. | 2. Vitu mbali mbali vinavyohusiana na duka.<br>3. Chati ya sarafu | |

# MWAKA WA PILI

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| 1. MAUMBO<br>(a) Maumbo Bapa (2D) | Mtoto aweze Kuunganisha maumbo (2D) | 1. Kwa kutumia mbinu ya onesho mwalimu awaongoze watoto kuunganisha maumbo (aina moja na aina tofauti).<br>2. Kwa kutumia mbinu ya michoro mwalimu awaongoze watoto kuunganisha maumbo.<br>3. Kwa kutumia mbinu ya mazoezi mwalimu awaongoze watoto kulinganisha maumbo. | 1. Chati ya maumbo yaliyounganishwa maumbo yaliokatwa/ Chati mguso.<br>2. Mchanga, vijiti, mbao ndogo ndogo, mkasi, gundi.<br>3. Madaftari ya kuandikia | 6 |
| (b) Maumbo Magumu.(3D) | Mtoto aweze Kutaja maumbo magumu (3D). | 1. Kwa kutumia mbinu ya onesho mbinu mwalimu awaongoze watoto kutaja maumbo magumu<br>2. Kwa kutumia mbinu ya maswala na majibu mwalimu awaongoze watoto kutaja maumbo kwenye maumbo magumu. .<br>3. Kwa kutumia mbinu ya kuchora | 1. Vitu mbali mbali vya maumbo ya 3D<br>2. Penseli<br>3. Penseli za rangi/krayons<br>4. Udongo wa ufinyanzi | 6 |
| | | mwalimu awaongoze watoto | | |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | kuchora maumbo magumu (3D). | | |
| 2. VIPIMO<br>(a) Urefu. | Mtoto aweze<br>Kupima urefu kwa kutumia vipimo tofauti vya asili. | 1. Kwa kutumia mbinu ya nyimbo mwalimu awaongoze watoto kuimba nyimbo ya urefu na ufupi.<br>2. Kwa kutumia mbinu onesho mbinu mwalimu awaongoze watoto kupima urefu kwa kutumia vipimo tofauti.<br>3. Kwa kutumia mbinu ya mazoezi mwalimu awaongoze watoto kupima urefu wa vitu kwa kutumia vipimo tofauti. | 1. Chati yenye vitu tofauti/chati mguso<br>2. Kamba<br>3. Nyanda<br>4. hatua<br>5. Pima | 6 |
| | (ii) Kupima masafa kwa kutumia vipimo vya asili.<br>(masomo ya nje ya darasa-out door class) | 1. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kupima masafa kwa vipimo mbali mbali vya asili kwenye mazingira ya skuli nje ya darasa.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya mazoezi mwalimu awaongoze watoto | 1. Chati inayoonesha vifaa na viungo vya kupimia masafa/ chatimguso.<br>2. Kamba.<br>3. Hatua.<br>4. Nyanda<br>5. Pima. | 12 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | kupima masafa kwa vipimo mbali mbali vya asili kwenye mazingira ya skuli nje ya darasa.<br>3. Kwa kutumia mbinu ya mchezo mwalimu awaongoze watoto kupima masafa kwa kutumia vipimo mbali mbali vya asili (mbio za masafa , hatua/pima 50) | | |
| (b) Uzito. | Mtoto aweze Kutofautisha vitu vizito na vyepesi. | 1. Kwa kutumia mbinu ya kuonesha mwalimu awaongoze watoto kutofautisha vitu vizito na vyepesi<br>2. Kwa kutumia mbinu ya mchezo mwalimu awaongoze watoto kutofautisha vitu vizito na vyepesi<br>3. Kwa kutumia mbinu ya mazoezi mwalimu awaongoze watoto kutofautisha vitu vizito na vyepesi. | 1. Chati inayoonesha mizani tofauti za kupimia/ Chati mguso<br>2. Vitu vya dukani<br>3. Chombo cha kupimana (see saw).<br>4. Spiringi<br>5. Mipira/rababendi | 6 |
| (c) Ujazo | Mtoto aweze Kupima ujazo kwa kutumia vitu tofauti. | 1. Kwa kutumia mbinu ya onesho mwalimu awaongoze watoto kupima ujazo kwa kutumia vitu | 1. Chati ya vitu mbali mbali vinavyotumika kwa ujazo wa | 6 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | tofauti.<br>2. Kwa kutumia mbinu mchezo mwalimu awaongoze watoto kupima ujazo kwa kutumia vitu tofauti.<br>3. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kupima ujazo kwa kutumia vitu tofauti. | vitu/chati mguso.<br>2. Maji.<br>3. Mchanga.<br>4. Chupa za plastiki.<br>5. Vikopo<br>6. Beseni la kutilia maji. | |
| 3. WAKATI<br>(a) Ratiba ya Siku. | Mtoto aweze<br>Kutaja ratiba ya siku | 1. Kwa kutumia mbinu ya nyimbo mwalimu awaongoze watoto kuimba kwa kutaja ratiba ya siku.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya onesho mfano mwalimu awaongoze watoto kutaja ratiba ya siku..<br>3. Kwa kutumia mbinu ya igizo mwalimu awaongoze watoto kutaja ratiba ya siku.<br>4. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze | 1. Saa bandia<br>2. Chati/chati Mguso<br>3. Saa halisi | 9 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | watoto kutaja ratiba ya siku. | | |
| (b) Miezi katika Mwaka. | Mtoto aweze<br>Kutaja miezi katika mwaka kwa mtiririko | 1. Kwa kutumia mbinu ya nyimbo mwalimu awaongoze watoto kutaja miezi katika mwaka.<br>2. Kwa kutumia mbinu onesho mbinu mwalimu awaongoze watoto kutaja miezi katika mwaka kwa mtiririko.<br>3. Kwa kutumia mbinu ya mchezo mwalimu awaongoze watoto kutaja miezi katika mwaka kwa mpango. | 1. Redio.<br>2. CD.<br>3. Kalenda.<br>4. Kadi.<br>5. Sinema boksi.<br>6. Chati/chati mguso. | **9** |
| (a) Mtiririko wa Matukio katika Mwaka. | Mtoto aweze<br>Kutaja matukio mbali mbali yanayotokea katika mwaka. | 1. Kwa kutumia mbinu ya igizo mwalimu awaongoze watoto kutaja matukio mbali mbali yanayotokea katika mwaka.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya kusimulia hadithi mwalimu awaongoze watoto kutaja matukio mbali mbali yanayotokea katika mwaka. | 1. Kalenda.<br>2. Sinema boksi.<br>3. CD.<br>4. Chati /chati mguso. | 9 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | 3. Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kutaja matukio mbali mbali yanayotokea katika mwaka (sherehe mbali mbali na matukio ya kitaifa | | |
| 4. FEDHA<br>(a) Noti. | Mtoto aweze:<br>(i) Kutaja aina za noti za fedha ya anzania | 1. Kwa kutumia mbinu ya onesho mbinu mwalimu awaongoze watoto kutaja aina za noti.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya mchezo mwalimu awaongoze watoto kutaja aina za noti. | 1. Chati yenye kopi za noti halisi/chati mguso.<br>2. Noti halisi. | 9 |
| | (ii) Kutumia noti za fedha ya Tanzania | 1. Kwa kutumia mbinu ya kuonesha, mwalimu awaongoze watoto kuhesabu 51—100 kwa mtiririko.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya mchezo, mwalimu awaongoze watoto kuhesabu 51—100. | 1. Vitu mbali mbali vya dukani.<br>2. Kopi za noti.<br>3. Noti mfano.<br>4. Chati yenye kuonesha noti mfano | |
| 5. NAMBARI<br>(a) Kuhesabu | Mtoto aweze<br>(i) Kuhesabu nambari | 1. Kwa kutumia mbinu ya kuonesha mwalimu awaongoze | 1. Chati ya nambari/mguso | 14 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| Nambari<br>51 - 100 | 51 – 100 (kwa awamu) | watoto kuhesabu nambari 51 – 100 kwa mtiririko.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya mchezo mwalimu awaongoze watoto kuhesabu nambari 51 – 100. | 2. Kadi za nambari/mguso<br>3. Abakasi<br>4. Vitu vya kuhesabia.<br>5. Kadi za kukata za samaki wenye nambari. | |
| | (ii) Kupanga nambari | Kwa kutumia mbinu ya mchezo mwalimu awaongoze watoto kupanga nambari kwa mtiririko. | Kadi za nambari/mguso | |
| (b) Kusoma Nambari 51 – 100. | Mtoto aweze Kusoma nambari 51 – 100.(kwa awamu) | 1. Kwa kutumia mbinu ya onesho mwalimu awaongoze watoto kuandika nambari | 1. Kadi za numerali | 6 |
| | (ii) kupanga nambari kwa muala kutoka ndogo kwanda kubwa.(51—100). kwa awamu | Kwa kutumia mbinu ya michezo, mwalimu awaongoze watoto kupanga nambari. kwa muala kutoka ndogo kwenda kubwa | Kadi za numerali | |
| (c) Kuandika Nambari | Mtoto aweze | Kwa kutumia mbinu ya mazoezi | 1. Mabuku | 22 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| 51 - 100 | Kujumlisha na kutoa. | mwalimu awaongoze watoto kujumlisha na kutoa hesabu ndogo ndogo ( jawabu isiyozidi kumi kwa kutumia nambari). | 2. Kadi.<br>3. Vifaa mbali mbali vya kuhesabia.<br>4. Penseli. | |
| (d) Matendo ya Kihesabati | Mtoto aweze :-<br>(i) kujimlisha nambari (jibu lisilozidi kumi) | 1. Kwa kutumia onyesho mbinu, mwalimu awaongoze watoto kujumlisha nambari.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya mazoezi, mwalimu awaongoze watoto kujimlisha nambari. ( jawabu lisizidi kumi na kuandika jawabu)<br>. | 1 Vifaa mbali mbali vya kuhesabia<br>2 Chati/ chati mguso<br>3 Kadi za namabri.<br>4 Karatasi<br>, 5. Mabuku na penseli.<br>6 Abakasi | 12 |
| | (ii) Kutoa nambari (nambari ya kutoa isizidi kumi na yenye kutolewa pia isizidi kumi na kuandika jawabu) | 1. Kwa kutumia onyesho mbinu, mwalimu awaongoze watoto kutoa nambari.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya mazoezi, mwalimu awaongoze watoto kutoa nambari.<br>. | 1Vifaa mbali mbali vya kuhesabia<br>2Chati/ chati mguso<br>3Kadi za namabri.<br>4karatasi<br>5aamabuku na penseli.<br>6Abakasi | |